TAARIFA KWA UMMA

UFAFANUZI WA BEI ZA MAJI NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA NA EWURA KWA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA JIJINI MWANZA (MWAUWASA)

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA) imeanza rasmi kutekeleza Agizo la EWURA la kutoza bei mpya za maji zilizofanyiwa mabadiliko kuanzia tarehe 01 Julai, 2019. Mabadiliko ya bei hizi mpya za Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza zimeanza kutumika mara tu baada ya kuchapishwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali - GN Namba 486/2019 (kwa lugha ya Kiingereza) na GN Namba 490/2019 (kwa lugha ya Kiswahili) la tarehe 28 Juni, 2019.

1. MPANGO NA HATUA ZA KUFANYA MABADILIKO YA BEI ZA MAJI

Mpango huu wa mabadiliko ya bei mpya za maji ulifuata na kuzingatia hatua mbalimbali katika kuwahusisha wadau wa huduma za maji na usafi wa mazingira kwa mujibu wa maelekezo ya mwongozo wa EWURA wa maombi ya kufanya mabadiliko ya bei za maji kama ifuatavyo:

a) Kabla ya MWAUWASA kuwasilisha EWURA mapendekezo ya kufanya mabadiliko ya bei, ilipewa kibali na Wizara ya Maji cha kuendelea na hatua za kuwasilisha EWURA maombi ya kuongeza bei za huduma ya majisafi na usafi wa mazingira.
b) Mara baada ya kupewa kibali na Wizara, mnamo tarehe 15/01/2019, MWAUWASA iliitisha kikao cha Wenyeviti wa Serikali za mitaa Jijini Mwanza, Baraza la watumiaji wa huduma za maji (EWURA CCC) na makundi ya wateja wanaotumia huduma mbalimbali za majisafi na usafi wa mazingira. Wadau hawa walielezwa bayana nia, umuhimu na uhalisia wa kufanya mabadiliko ya bei za maji iliyolenga kuboresha huduma za majisafi na usafi wa mazingira Jijini Mwanza ambapo wadau wote walioalikwa waliridhia na kukubaliana na mpango wa MWAUWASA kufanya mabadiliko ya bei za maji.

c) Baada ya makubaliano hayo ya wadau, tarehe 19 Januari 2019, MWAUWASA iliwasilisha rasmi EWURA maombi yake ya kufanya mabadiliko ya bei za majisafi na usafi wa mazingira.

d) Tarehe 28 Machi 2019, EWURA waliitisha mkutano na wananchi (wakiwemo madiwani, viongozi wa serikali za mitaa, watendaji wa mitaa, na wateja wa makundi yote ya watumiaji maji kwa ajili ya kufanya Taftishi (Public inquiry) kwa kuyaweka wazi kwa umma maombi ya MWAUWASA ya kuongeza bei za maji. Mkutano huu wa Taftishi pia ulihusisha Baraza la Ushauri la Serikali lililopitia maombi ya bei za maji na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Maji la EWURA (EWURA CCC).

e) Baada ya hatua zote hizo kufanyika na kwa kuzingatia pia maoni na ushauri mbalimbali kutoka kwa wadau wote waliotajwa katika hatua hizo hapo juu, tarehe 29 Mei, 2019 EWURA iliidhinisha na kutoa agizo (tariff order) la marekebisho ya bei mpya kwa MWAUWASA.

f) Bei hizi mpya zilitangazwa kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 28 Juni, 2019 kwamba zianze kutumika tarehe 01 Julai, 2019.

Kwa mujibu wa Agizo la EWURA bei mpya zilizoidhinishwa kutozwa na MWAUWASA zimeambatana na masharti (conditions) sita (6) ambayo yanapaswa kutekelezwa na MWAUWASA. Masharti haya yamezingatia maoni na ushauri kutoka kwa wadau wote walioshirikishwa.

2. LENGO LA KUFANYA MABADILIKO YA BEI ZA MAJI

Lengo la kufanya mabadiliko haya ya bei za majisafi na usafi wa mazingira ni kama ifuatavyo:

a) Kujenga miradi mipya yenye kuongeza mtandao wa usambazaji maji ili kuyafikia maeneo yanayokosa maji na yanayopata maji kidogo.
b) Kuongeza mitandao ya mfumo wa uondoshaji majitaka kwenye maeneo ambayo hayana mfumo wa majitaka
c) Kufanya matengenezo na ukarabati wa mabomba ya wateja yanayosababisha mivujo ya maji bila kuwatoza gharama za matengenezo na ukarabati.
d) Kukabiliana na gharama kubwa za uendeshaji zinazotokana na watoa huduma za manunuzi ya madawa ya kutibu maji, mabomba na viungio,

matengenezo ya vipuli vya mitambo mikubwa na gharama kubwa za umeme wa kuendesha mitambo.

Ikumbukwe kwamba, mara ya mwisho EWURA iliidhinisha mabadiliko ya bei za maji kwa MWAUWASA takribani miaka minne iliyopita. Kwa kipindi chote hicho, MWAUWASA imeendelea kutumia bei zile zile licha ya kuwepo kwa mabadiliko ya gharama mbalimbali za watoa huduma kama ilivyoelezwa hapo juu. Ongezeko la gharama hizi kubwa za uendeshaji zimesababisha MWAUWASA kushindwa kutekeleza mipango yake ya kuwafikishia huduma ya maji kikamilifu wananchi walio katika maeneo yenye changamoto za uhaba wa maji katika Jiji la Mwanza na viunga vyake.

Baadhi ya maeneo ambayo yamekuwa na changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji ambayo MWAUWASA imekusudia kuboresha huduma hii ni pamoja na Kisesa, Bujola, Buhongwa, Kiseke, Nyasaka Islamic, Nyasaka Riverside, Ibanda, Buswelu, Nyamhongolo, Kishiri, Nyegezi Kalifonia, Ihila, Mwashi, Shadi, Bugarika, Nyakurunduma, Mabumbani, Mahina, Tambuka Reli na maeneo mengine yaliyo kwenye miinuko Jijini Mwanza. Hata hivyo, pamoja na miradi yake ya ndani, MWAUWASA imekuwa ikisimamia pia utekelezaji na uboreshaji wa huduma ya maji kupitia miradi ya maji inayotekelezwa katika maeneo ya wilaya zote mbili za Ilemela na Nyamagana, miradi ambayo awali ilikuwa ikitekelezwa na Halmashauri za wilaya husika. Maeneo haya ni pamoja na Nyamwilolelwa, Shibula, TX, Igombe, Igogwe, Nyafula, Kabusungu, Ilalila, Sangabuye, Kahama, Nyamadoke, Masemele, Isela, Lukobe, ilekako, Isesabudaga, Lwanima na Fumagila.

3. BEI ZA MAJI NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA NA EWURA

Majedwali yafuatayo yanainisha bei za maji na tozo zilizoidhinishwa na EWURA zianze kutumika rasmi kuanzia Julai 2019:

Jedwali Na.1: Bei za Maji Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi/ Mita ya Ujazo)

Kundi la Mteja	Kiwango cha Matumizi kwa Kila Mita ya Ujazo (m^3)	Bei za Zamani (TZS/m^3)	Bei Zilizoidhinishwa (TZS/m^3)		
		2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani	Kundi Na. 1: <=10 m^3	700	1,225	1,345	1,345
	Kundi Na. 2: 11 – 25m^3	865	1,515	1,665	1,665
	Kundi Na 3: >25 m^3	900	1,575	1,730	1,730
Taasisi		925	1,620	1,780	1,780
Biashara		1,345	2,355	2,585	2,585

Viwanda		1,680	2,945	3,230	3,230
Ujenzi		1,680	2,945	3,230	3,230
Viwanda vya Vinywaji vya chupa		2,850	3,930	4,405	6,155
Magati		500	875	960	960

Muhimu: Kundi Na.1 ni la wateja wenye mita za maji wanaotumia maji kati ya mita za ujazo 1 hadi 10 ambapo mita moja ya ujazo ni sawa na lita 1,000 za maji ambazo ni sawa na ndoo 50 za lita 20). Kwa lugha nyingine ni wale wanaotumia maji kati ya lita 1,000 hadi lita 10,000 za maji. Kwa mfano, kwa bei ya zamani kwa mita moja ya ujazo ambayo ni sawa na lita 1,000 za maji au ndoo 50 za maji, kwa matumizi ya kundi Na.1 hapo juu ilikuwa Tshs. 700/= kwa kila mita moja ya ujazo (sawa na Tshs.14 kwa kila ndoo ya maji). Kwa bei ya sasa iliyoongezeka kuanzia Julai 2019, mita moja ya ujazo ambayo ni sawa na lita 1,000 au ndoo 50 za maji imekuwa Tshs.1,225 kwa kila lita 1,000 za maji au kwa kila ndoo 50 za maji (sawa na Tshs.24.50 kwa kila ndoo ya maji). Kwa hiyo utaona kwamba ukilinganisha bei ya zamani na bei ya sasa kwa ndoo kwa wateja wenye mita za maji katika Kundi hili imeongezeka kwa Tshs.10.50 tu kutoka Tshs.14 hadi Tshs.24.50 kwa ndoo moja ya maji. Utaratibu ni huu huu kwa makundi mengine ya wateja yanayofuata.

Jedwali Na.2: Bei Zilizoidhinishwa za Majitaka

Kundi la Mteja	Kiwango cha Matumizi (m^3)	Bei za Zamani (TZS/m^3)	Bei Zilizoidhinishwa (TZS/m^3)		
		2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani	Kundi Na. 1: <=10 m^3	305	615	675	675
	Kundi Na. 2: 11 – 25m^3 m^3	330	760	835	835
	Kundi Na. 3: >25 m^3	390	790	865	865
Taasisi		395	810	890	890
Biashara		575	1,180	1,295	1,295
Viwanda		720	1,475	1,615	1,615
Ujenzi		720	1,475	1,615	1,615
Viwanda vya Vinywaji vya chupa		1,220	2,495	2,740	2,740

Jedwali Na.3: Tozo Zilizoidhinishwa za Kuondoa Majitaka (TZS/Tripu)

Kundi la Mteja	Tozo za Zamani	Tozo Zilizoidhinishwa		
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Kundi Na 1 (Boza la Ujazo wa 6m^3)	50,000	102,000	102,000	102,000
Kundi Na. 2 (Boza la Ujazo wa 8m^3)	60,000	136,000	136,000	136,000
Kundi Na. 3 (Boza la Ujazo wa 10m^3)	70,000	170,000	170,000	170,000

Jedwali Na.4: Tozo za Huduma Zilizoidhinishwa (TZS/Mwezi)

Kundi la Mteja	Tozo za Zamani (TZS/Mwezi)	Tozo Zilizoidhinishwa (TZS/Mwezi)		
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani	2,100	Tozo ya Huduma Haitaruhusiwa		
Taasisi	3,000			
Biashara	3,000			
Viwanda	9,000			
Ujenzi	9,000			
Viwanda vya Vinywaji vya chupa	9,000			

Jedwali 5: Ada Iliyoidhinishwa ya Maunganisho Mapya (TZS/Unganisho)

Kundi la Mteja	Ada ya Zamani	Ada Iliyoidhinishwa		
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani	Asilimia ishirini ya gharama za maunganisho kama inavyojieleza katika Kifungu cha 24 cha Kanuni za Maji za 2013	Asilimia ishirini ya gharama za maunganisho kama inavyojieleza katika Kifungu cha 24 cha Kanuni za Maji za 2013		
Taasisi				
Biashara				
Viwanda				
Ujenzi				
Viwanda vya Vinywaji vya chupa				

Jedwali Na.6: Ada Iliyoidhinishwa ya Marejesho ya Huduma ya Maji Baada ya Kukatiwa (TZS/Rejesho)

Kundi la Mteja	Ada za Zamani	Ada Zilizoidhinishwa		
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani	10,000	15,000	15,000	15,000
Taasisi	15,000	15,000	15,000	15,000
Biashara	20,000	15,000	15,000	15,000
Viwanda	25,000	15,000	15,000	15,000
Ujenzi	25,000	15,000	15,000	15,000
Viwanda vya Vinywaji vya chupa	25,000	15,000	15,000	15,000
Magati	10,000	15,000	15,000	15,000

Jedwali Na.7: Ada Zilizoidhinishwa za Maunganisho Mapya ya Majitaka (TZS/Unganisho)

Kundi la Mteja	Ada za Zamani	Ada Zilizoidhinishwa		
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Makundi yote ya Wateja	5,000	5,000	5,000	5,000

Jedwali Na.8: Ada Zilizoidhinishwa za Kumwaga Majitaka (TZS/m^3)

Kundi la Mteja	Ada za Sasa	Ada Zilizoidhinishwa		
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Makundi yote ya Wateja	-	1,700	1,700	1,700

Jedwali Na.9: Tozo Zilizoidhinishwa za Huduma ya Maji kwa Maboza (TZS/m^3)

Kundi la Mteja	Tozo za Zamani	Tozo Zilizoidhinishwa		
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Makundi yote ya Wateja	-	11,510	13,178	13,178

IMETOLEWA NA OFISI YA UHUSIANO
MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA JIJINI MWANZA
(MWAUWASA)
06 Agosti, 2019.